

NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU
IDARA YA UANDISHI
1 Januari 2023

Kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa

Wapendwa Marafiki wa Kibaha'i,

Kwa kuzingatia hali ya kiusalama katika eneo hili na uzoefu husika wa baadhi ya wageni, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imetuomba tuwawasilishie ifuatavyo.

Ni sera ya muda mrefu ya Makao Makuu ya Kibaha'i ya Ulimwengu kwamba waumini wanaoishi moja kwa moja au kwa angalau sehemu ya mwaka nchini Iran, bila kujali utaifa wao, wasingeweza kuja Nchi Takatifu kwa ziara au hija fupi. Sasa, kutokana na msimamo mkali wa kiusalama wa serikali za eneo hili, imekuwa lazima, kwa kipindi fulani, kuwaomba Wabahá'í wote ambao wameishi au kutembelea kwenye chimbuko la Imani, hata kwa muda mfupi, kutokuja Israel kwa sababu yoyote ile hadi angalau miaka mitano imepita tangu ziara yao ya mwisho nchini Iran. Tafadhalini wajulisheni marafiki katika jumuiya zenu kuhusiana na hatua hii kwa jinsi muonavyo inafaa.

Tunasikitika sana kwa ukatishaji na uvunjaji huu wa moyo ambao baadhi ya marafiki bila shaka, watapitia, kama matokeo ya hatua hii ya lazima, na inatumainiwa kwa shauku kwamba muda si mrefu zuiyo hili linaweza kuondolewa. Mahujaji watarajiwa na wageni wa muda mfupi ambao wamekuwa Iran kwa miaka mitano iliyopita wanaombwa kuwasiliana na Idara ya Hija ili kupanga upya safari zao.

Pamoja na salaam za upendo wa Kibahá'í,

Idara ya Uandishi

Nakala: Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa
Bodi za Washauri
Washauri